**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA KATIKA SHULE ZA SEKONDARI ZA SERIKALI TANZANIA

**November, 2025**

**Dodoma**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS – TAMISEMI**

Mkuu wa Shule 0752-916826/ 0655681626

Matron 0625369078/ 0621470144

Shule ya Sekondari DR. Samia S.H

S.L.P. 59, TUNDUMA

Tarehe 22/11/2025

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi …………**

**……………………………………………..**

**S.L.P ……………………………………..**

**……………………………………………..**

Yah: **MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA KATIKA SHULE YA SEKONDARI DR. SAMIA S.H. HALMASHAURI YA MJI TUNDUMA MKOA WA SONGWE MWAKA 2026**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Kwanza katika Shule hii mwaka 2026.

Shule ya Sekondari **DR. Samia S.H** ipo umbali wa Kilometa 12 Kaskazini mwa Mji wa Tunduma. Usafiri wa daladala kutoka standi kuu ya mabasi ya Mji wa Tunduma, nauli ni Shilingi 700/= hadi chapwa standi. Pia utapanda Pikipiki kutoka chapwa mpaka mtaa wa namole shuleni-Dkt Samia S.H kwa nauli ya Shilingi 5000/=.

Muhula wa Masomo utaanza tarehe 13.01.2026, hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe 12.01.2026. Mwisho wa kuripoti ni tarehe 23.01.2026

## 2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-

### 2.1 Sare za Shule

i. Sare za shule hii ni sketi za vitambaa vya draft zenye mshono wa rinda box mbele na nyuma, pembeni kulia na kushoto malinda manne ya kawaida na iwe ndefu kufikia kwenye kiwiko cha mguu. Rangi ya kitambaa cha sketi imeambatishwa kwenye fomu hii. Endapo kutakua na changamoto yoyote katika upatikanaji wa sare hizo wasiliana na uongozi wa shule

ii. Mashati mawili, meupe ya mikono mifupi aina ya tomato. Nendo itabandikwa shuleni kwa shilingi elfu mbili.

iii. Kwa waislam watavaa hijab ya rangi nyeupe inayofunika kifua cha mwanafunzi, pia iwe ndefu kufikia kifundo cha mkono akisimama. (Aje nazo mbili)

iv. Trucksuit mbili, moja ya dark bluu na nyengine ya kijivu zenye mistari ya rangi nyeupe pembeni na raba nyeusi jozi moja.

v. Tisheti (T-shirt) mbili za rangi ya kijivu na dark bluu zenye mistari meupe kwa pembeni. Maandishi na Nembo kwenye T-sheti itawekwa shuleni kwa shilingi elfu tano.

vi. Viatu vya shule ni jozi mbili nyeusi vya kufunga na kamba venye visigino vifupi aje navyo

vii. Soksi jozi mbili nyeupe ndefu, sweta la shule jozi mbili nyeusi yenye shingo ya V na mkono mirefu. Aje nazo.

viii. Nguo za kushindia ***shamba dress*** rangi ya zambarau yenye mshono wa solo na iwe ndefu kuvuka magoti usawa wa kiwiko cha mguu. Aje nayo

### 2.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-

i. Madaftari tisa(09) makubwa (Q3 AU Q4) pamoja na madaftari tisa madogo aiana ya msomi kwa ajili ya mazoezi

ii. Ream paper ya Karatasi Mbili kwa mwaka

iii. Vitabu vya masomo husika

iv. Godoro lenye ukubwa wa ft 2.5x6

v. Mashuka Jozi 2 yenye rangi ya pink na bluu bahari, blanket 1, foronya ya godoro 1, chandarua 1 nyeupe.

vi. Nguo za ndani za kutosha.

vii. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe) rangi ya pink

viii. Ndoo 2 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko na tambara deki

ix. Kwanja 1

x. Mfagio 1 (hard broom)

xi. Reki 1 au jembe

xii. Sabuni ya maji kwa ajili ya usafi

xiii. Dumu la lita tano kwa ajili ya kutunzia maji ya kunywa

**NB: KILA MWANAFUNZI MWENYE BIMA YA AFYA YA TAIFA (NHIF) AJE NAYO NA KAMA HANA AJE NA SHILINGI ELFU HAMSINI NA MIA NNE TU (50,400/=) ILI KUPATA BIMA YA AFYA YA TAIFA.**

## 3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation)
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote
ix. Kutunza mali za shule
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- ❖**Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**
- ❖**Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**
- ❖**Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa).**

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**4. Viambatisho na Fomu Muhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

**5.** Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

**Saini ya Mkuu wa Shule** ..........................................

**Jina la Mkuu wa Shule** ....ANNA S. MUSHI....

**Mhuri wa Mkuu wa Shule** ..........................................

MKUU WA SHULE SHULE YA SEKONDARI DR SAMIA S.H S.L.P 59 TUNDUMA

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPOUJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO:**

- **Mkuu wa shule 0752916826**
- **Makamu Mkuu wa Shule 0746620939**
- **mwalimu Mwandamizi Taaluma 0658428454**
- **mwalimu Mwandamizi Malezi 0766927850**

## UTHIBITISHO WA URAIA WA MTANZANIA

Nadhibitisha kuwa..................................................................... (jina kamili la mwanafunzi) ni raia wa Tanzania kwa kuzaliwa/kwa kuandikishwa

Baba yake (jina kamili) ..................................................................

Amezaliwa katika mkoa wa ................................ Wilaya ya ...........................

Tarafa ya ...............................Kata ya ........................................

Mama yake (jina kamili) ..............................................................

Amezaliwa katika kata ya ............................ Wilaya ya ...............................

..........................................................................

**Mkuu wa Wilaya**

**NB**: kila mwanafunzi atalazimika kuishughulikia hati kikamilifu. Ikishajazwa irudishwe kwa Mkuu wa shule siku ya kuripoti shuleni. **Au leta nakala ya cheti cha kuzaliwa badala ya fomu hii**.

**PRESIDENT'S OFFICE**

**REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**

DR. SAMIA S.H. SECONDARY SCHOOL

P.O. Box 59

**TUNDUMA.**

Date: ....................................

To:

**THE MEDICAL OFFICER,**

...........................................

...........................................

Please examine ......................................................................

As to her fitness for pursuing further education at this school.

- Hemoglobin ..............................................
- P.V. Blooding...............................................
- (A) Blooding ..............................................

  (B) Hearing ..............................................
- Blood Pressure..........................................
- Urine for Sugar and Pregnancy tests............................
- Stool for routine examination..........................................
- Asthma ..............................................................
- Skin diseases ..........................................................
- Leprosy ..................................................................
- Pulmonary tuberculosis ..............................................
- Employs ..............................................................
- Deformity ......................................................
- Mental problem...................................................
- Comments

.........................................................................................................

**.....................................................**

**DESIGNATION**

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**
**HALMASHAURI YA MJI TUNDUMA**
**SHULE YA SEKONDARI DR. SAMIA S.H.**
FOMU YA KUKUBALI NAFASI

**a. TAARIFA BINAFSI ZA MWANAFUNZI (ijazwe na mwafunzi mwenyewe)**

Jina kamili[kama alivyo sajiliwa darasa la saba]..........................................................

Tarehe ya kuzaliwa...................Kabila.....................dini na dhehebu........................

shule nitokayo...........................Mahali niishipo...............................

Mkoa.............................Anuani...............................................

Jina la baba/mlezi..............................................kazi yake...............................

Jina la mama/mlezi...........................................kazi yake................................

Wazazi/walezi wanaishi (wapi).............................pamoja/au wametengana..............

Anuani ya mzazi/mlezi...............................simu.........................................

Wakati wa likizo nitakuwa kwa (mtaje)................................wapi..........................

Nathibitisha kuwa taarifa nilizotoa hapo juu ni za kweli na sahihi;

Sahihi ya mwanafunzi...................................tarehe...................................

KUKUBALI (mwanafunzi mwenyewe ajaze)

Mimi...................................................................................nimesoma maagizo kwa makini na kuzielewa taratibu za shule na nipo tayari kuzifuata. Hivyo ninakubali nafasi niliyopewa na nitafika shuleni tarehe iliyopangwa.

**b. IJAZWE NA MZAZI AU MLEZI**

Mimi……………………………………………………………. ambaye ni ……………………. wa mwanafunzi huyu nimesoma kwa makini maelekezo pamoja na sheria za shule katika fomu ya kujiunga. Nipo tayari ajiunge na shule hii, naahidi kumpa mahitaji yote ili aweze kupata elimu yake vizuri katika shule hii. Aidha nitasaidiana na walezi wa shuleni katika kumlea mwanafunzi huyu katika maadili mema na kuitikia wito wa kufika shuleni pale nitakapohitajika.

Anuani yangu ya kudumu…………………………..simu………………………………

Nikipata uhamisho ama kubadilisha makazi nitaijulisha shule kwa maandishi.

Nathibitisha Taarifa nilizotoa ni sahihi na kweli

Sahihi ya mzazi /mlezi……………...











